# TAARIFA YA MAFANIKIO YA SKIMU YA UMWAGILIAJI MOMBO

## 1 UTANGULIZI

Skimu ya Umwagiliaji Mombo ni moja ya skimu za mfano hapa nchini. Skimu hii iko kwenye Bonde la Mkomazi *(Lower Mkomazi Valley)* katika Tarafa ya Mombo, wilayani Korogwe katika mkoa wa Tanga. Chanzo cha maji ya umwagiliaji ni mto Soni unaoanzia katika milima ya Usambara wilayani Lushoto.

## 2 HISTORIA YA SKIMU

Skimu ya Umwagiliaji Mombo ilianzishwa mwaka 1967 ikiwa na miundombinu ya asili *(Traditional Irrigation System)*.

Mwaka 1979 skimu hiyo iliandikishwa kama chama cha ushirika na kupewa namba ya usajili 2207 kikiwa na wanachama waanzilishi wapatao 40. Kuanzia hapo chama kimekuwa kikijiendesha kama chama cha ushirika ambacho kwa sasa kina wanachama 300.

Mwaka 19978/1979, Serikali ya Ujerumani ikishirikiana na Serikali ya Tanzania, kupitia mradi uliojulikana kama *Tanga Integrated Rural Developmnet projct (TIRDEP)*, ilijenga banio la kisasa *(intake)*, ilikarabati mifereji mikuu, ilijenga bwawa dogo la kuhifadhia maji wakati wa usiku *(night storage reservoir)* na kusawazisha mashamba *(farm leveling)*.

Mwaka 1993 Skimu ya Mombo ilikumbwa na mafuriko makubwa ambayo yaliharibu baadhi ya miundombinu ya umwagiliaji jambo ambalo lilipelekea Serikali kuboresha tena maeneo yaliyoathiriwa na mafuriko hayo. Maeneo yaliyokarabatiwa ni Banio kuu, mifereji mikuu, bwawa la kuhifadhia maji, n.k.

Mwaka 2000/2001 serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula chini ya mradi wa RBM-SIIP iliboresha maeneo yaliyoathiriwa na mafuriko ikiwa ni pamoja na kujenga tuta la kuzuia mafuriko *(flood protection bund)* kwa fedha zilizopatikana toka benki ya Dunia *(World Bank)*. Tangu wakati huo skimu imekuwa ikiendelea vizuri.

Skimu ya Umwagiliaji Mombo inayo hati ya kutumia maji *(water use permit)* kutoka mto Soni kiasi cha lita 268.85 kwa sekunde yenye namba ya usajili 2508 iliyotolewa na Ofisi ya Maji Bonde la Pangani mwaka 1997.

## 3 ENEO LA SKIMU

Skimu hii ina ukubwa wa hekta mia mbili na ishirini (220 ha) ambazo zimegawanyika katika sehemu kuu mbili:

- Shamba ‘A’ – hekta mia moja (100 ha);
- Shamba ‘B’ – hekta mia moja na ishirini (120 ha).

Eneo lote linalimwa katika mzunguko wa misimu mitatu kwa mwaka kama ifuatavyo:

(i) Msimu wa Januari - Juni - 100 ha;
(ii) Msimu wa Julai - Desemba - 120 ha;
(iii) Msimu wa Septemba - Machi - 100 ha.

Wakulima wanaonufaika na Skimu ya Mombo ni 429 (Wanawake 233 na Wanaume 196) ambao kila mmoja anamiliki ekari moja na robo (1.25 *acre*). Wakulima hawa wanatoka katika vijiji vya Mombo, Jitengeni, Mlembule na Mwisho wa Shamba.

## 4 UZALISHAJI WA MAZAO

Zao kuu ambalo linalimwa kwenye skimu kwa muda mrefu ni mpunga, aidha mazao kama mahindi na jamii ya mikunde yamekuwa yakilimwa pale uhaba wa maji unapojitokeza.

Zao la mpunga ambalo hulimwa katika eneo kubwa la skimu, uzalishaji wake umekuwa ukiongezeka msimu hadi msimu. Kwa mfano wastani wa uzalishaji kwa sasa ni tani sita kwa hekta moja (6 tani/ha), ingawa baadhi ya wakulima *(key farmers)* wameweza kufikia uzalishaji wa tani kumi kwa hekta (10 tani/ha) kutegemea na hali ya hewa na upatikanaji wa maji.

## 5 UTUNZAJI NA UENDESHAJI WA SKIMU

Wakulima wa skimu ya Mombo wamejiwekea utaratibu wa utunzaji na uendeshaji wa skimu yao ili kuhakikisha kuwa miundombinu iliyojengwa na serikali inakuwa endelevu na wamejiwekea utaratibu kama ifuatavyo:

(i) **Kazi za kujitolea za msaragambo *(Communal Works)*:** Hapa upo utaratibu kwa wakulima wote siku mbili kila wiki (Jumatatu na Alhamisi) kujitolea kufanya usafi wa mifereji mikuu, barabara na ukarabati wa miundombinu mbalimbali.

(ii) **Michango ya wakulima (fedha taslimu)**: Wakulima wamejiwekea utaratibu wa kuchangia fedha taslimu Tshs. 24,000 kila msimu kwa ajili ya utunzaji na uendeshaji wa skimu tangu mwezi Novemba 2009 hadi Juni 2010.

## 6 ELIMU NA HUDUMA ZA UGANI KWA WAKULIMA

Wakulima wa skimu ya Mombo walipata fursa mbalimbali za kupata mafunzo ya kilimo bora cha mazao na matumizi bora ya maji kupitia:

- Wizara ya Kilimo na Chakula chini ya Mradi wa Kusimamia Matumizi Bora ya Raslimali ya Maji na Uboreshaji wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji mashambani cha Wakulima wadogo *(River Basin Management and Smallholder Irrigation Improvement Project – RBMSIIP)* katika mabonde ya mito Rufiji (ambapo skimu 7 ziliboreshwa) na Pangani (ambapo skimu 8 ziliboreshwa);

- Chuo cha KATC na Kituo cha Utafiti wa Udongo cha Taifa cha Mlingano kwa kushirikiana na maafisa ugani walioko kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe wamekuwa wakitoa elimu kwa wakulima kwa njia ya shamba darasa *(Farmer field schools)* juu ya uboreshaji wa rutuba ya udongo kwa kuzungusha zao la mpunga na jamii ya mikunde *(Dolichos lab-lab);*

- Mafunzo kuhusu aina na matumizi sahihi ya viwango vya mbolea za viwandani.

# 7 UONGOZI NDANI YA SKIMU

## 7.1 Chama cha Ushirika

Skimu ya Mombo ina chama cha Ushirika kinachoongozwa na Bodi yenye wajumbe tisa (9) wa kuchaguliwa kwa mujibu wa katiba ya Ushirika. Kati ya hao, wajumbe saba (7) ni wanaume na wawili (2) ni wanawake. Mgawanyo wa madaraka ni kama ifuatavyo:

- Mwenyekiti wa Bodi;
- Makamu Mwenyekiti;
- Wajumbe saba (7) kutoka ndani ya eneo la skimu.

Pia skimu ina wafakanyakazi wawili walioajiriwa na chama cha Ushirika ambao ni:

- Katibu wa Ushirika;
- Mhazini.

Majukumu ya Bodi ni kutekeleza mambo yafuatayo:

(i) Kusimamia shughuli zote za maendeleo ya Ushirika;
(ii) Kuwa wawakilishi wa maeneo wanakotoka;
(iii) Kubuni na kusimamia vyanzo vya mapato;
(iv) Kutafuta pembejeo na zana za kilimo kwa wakulima.

## 7.2 Kamati ndogo ndogo za utendaji

Zipo kamati ndogo ndogo za kiutendaji zilizoundwa kuisaidia Bodi kama ifuatavyo:

1. Kamati ya Mipango na Fedha: Kamati hii ina majukumu yafuatayo:

    - Kusimamia mapato na matumizi ya ushirika;
    - Kubuni vyanzo vya mapato;
    - Ununuzi wa pembejeo kwa ajili ya wakulima.

2. Kamati ya Miundombinu: Kamati hii ina majukumu yafuatayo:

    - Ukarabati wa miundo mbinu;
    - Usimamizi wa ratiba za maji.

3. Kamati ya Kilimo na Mazingira: Kamati hii ina majukumu yafuatayo:

    - Kusimamia shughuli zote za kilimo (kilimo bora cha mpunga);
    - Udhibiti wa wanyama waharibifu kwenye skimu.

### 7.3 Meneja wa Skimu

Skimu ya Mombo ina meneja ambaye ni mtumishi / mwajiriwa wa Serikali anayesimamia moja kwa moja shughuli za umwagiliaji na matumizi bora ya ardhi/ udongo na maji katika skimu. Kimsingi majukumu yake ni haya yafuatayo:

- Kusimamia/kuratibu shughuli zote za kitaalamu zinazofanyika kwenye skimu;

- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wakulima juu ya kilimo bora cha umwagiliaji;

- Kupanga kalenda za kilimo na ratiba za usambazaji maji;

- Kushirikiana na viongozi wa ushirika kusimamia shughuli zote za maendeleo ya ushirika;

- Kupokea majukumu / maagizo / maelekezo toka ngazi za juu na kuwafikishia wakulima;

- Kuandika taarifa ya maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji na kuwakilisha ofisi ya kilimo ya wilaya.

## 8 UMILIKI WA MASHAMBA NDANI YA SKIMU

Skimu hii inamilikiwa na Chama cha Ushirika cha Wakulima Wamwagiliaji Mombo *(Mombo Irrigation scheme agricultura cooperative Socity – MISACS).* Mtu anayetaka kulima ndani ya skimu hutakiwa kutuma maombi kwa kujaza fomu na kuwasilisha kwenye Ushirika. Maombi ya mkulima husika hujadiliwa na kama kuna eneo lililoko

wazi hupewa. Mtu asipozingatia taratibu na sheria ndogo ndogo zilizowekwa hunyang'anywa eneo na kupewa mwingine aliyeomba. Hata hivyo hivi sasa eneo lote limegawiwa wakulima.

## 9 MAFANIKIO YA SKIMU

Wakulima wa skimu ya Umwagiliaji Mombo wamepata mafanikio makubwa kupitia kilimo cha umwagiliaji kama ifuatavyo:

- Kupitia mafunzo mbalimbali yaliyotolewa kwa wakulima, uzalishaji wa mazao umeongezeka kutoka wastani wa tani 2 hadi 6 kwa hekta moja. Kutokana na mafanikio hayo skimu imeteuliwa kuwa ya mfano kwa skimu zingine zilizoko Kanda ya Umwagiliaji Kilimanjaro;

- Hali ya maisha ya wakulima imekuwa bora kutokana na uzalishaji wenye tija, mfano ujenzi wa nyumba bora, kulipia watoto karo, kununua vifaa vya mawasiliano (Simu, Luninga) n.k.;

- Wakulima wameweza kusambaza elimu kwa wakulima wengine ndani na nje ya nchi kama Uganda, Kenya, Malawi n.k.;

- Kuweza kutunza miundombinu ya umwagiliaji kwa kipindi kirefu;

- Skimu imeweza kuwapatia ajira wakulima wengi walioko kwenye eneo la mradi na maeneo ya jirani.

## 10 CHANGAMOTO ZILIZOPO

- Uhaba wa maji ya umwagiliaji, hii inatokana na kupungua kwa kiwango cha mvua inayonyesha msimu hadi msimu;

- Uwezo mdogo wa bwawa la kuhifadhia maji. Bwawa lililopo ni dogo halina uwezo wa kuhifadhi maji yanayoweza kutosheleza kipindi cha ukame (Kutokana na kujaa tope);

- Kutopatikana trekta za kukodi kwa wakati hususan kipindi cha masika husababisha wakulima kuchelewa kutayarisha mashamba yao ili kuendana na kalenda ya msimu;

- Kutokuwa na soko la uhakika la mazao.

## 11 JUHUDU ZA WAKULIMA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ZILIZOPO

- Kupanda mazao mbadala ambayo hayatumii maji mengi hususani kipindi cha ukame mfano mahindi, fiwi *(Dolichos lab-lab)*;

- Kuanzishwa kwa chama cha kuweka na kukopa (SACCOS) chenye wanachama mia moja hadi sasa;

- Kuanzisha utaratibu wa michango ya fedha taslimu kwa wakulima kwa lengo la kununua trekta;

- Kuomba toka Serikalini kupitia ofisi ya kilimo ya wilaya ndani ya mpango wa kuendeleza kilimo wilayani (DADPs) kuingizwa kwenye bajeti ili kuboresha bwawa lililopo.

## 12 MAPENDEKEZO YA WAKULIMA KWA SERIKALI KUHUSIANA NA CHANGAMOTO ZILIZOPO

- Serikali isaidie kujenga bwawa kubwa zaidi litakalokuwa na uwezo wa kuvuna maji ya mvua ili kilimo cha umwagiliaji kiendelee kuwa endelevu na cha uhakika;

- Serikali itoe mikopo yenye masharti nafuu na upatikanaji wa zana za kilimo kama matrekta makubwa na madogo kwa ajili ya kilimo.



**1. Ofisi ya Skimu ya Mombo**



**2. Banio la kisasa lililojengwa**



**3. Usafi wa mifereji unazingatiwa**



**4. Moja ya Vigawa maji vilivyojengwa**




**5. Bwawa dogo la kuhifadhi maji**



**6. Kuandaa kitaluu cha miche ya mpunga**



**7. Maumbo ya kugawanyia maji mashambani**




**8. Jiwe la msingi liliwekwa wakati wa Mbio za mwenge**



**9. Bwawa dogo la kuhifadhi maji**



**10. Kilimo cha mahindi nje ya skimu**



**11. Mchakato wa kujenga nyumba bora**



**12. Mafanikio yaliyopatikana yapelekea Ujenzi wa nyumba bora**



**9. Mama aliyefanikiwa kuvuna tani 10/ha**



**10. Mama huyo amejenga nyumba bora kutokana na mafanikio aliyoyapata**